JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

TAKUKURU KAGERA YAWAPANDISHA KIZIMBANI KUMI NA MBILI KWA WIZI WA ZAIDI YA SHILINGI MILIONI MIA NNE

TAARIFA KWA UMMA

FEBRUARI 05, 2021

Utangulizi

Ndugu wanahabari, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kagera tumeendelea kutekeleza majukumu yetu kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sheria namba 11 ya mwaka 2007. Katika utekelezaji wa majukumu yetu tumeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa mapambano dhidi ya Rushwa wakiwemo waandishi wa habari, viongozi wa serkali na wananchi kwa ujumla.

Ndugu wanahabari,

TAKUKURU Mkoa wa Kagera mwanzoni mwa mwaka jana, tulipokea maelekezo kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Kagera Mhe. Brig. Gen. Marco Elisha Gaguti akitutaka kufanya uchunguzi wa kina katika Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo kutokana na kuwepo kwa taarifa za wizi, ubadhilifu na ufujaji wa mapato ya ndani ya zaidi ya shilingi milioni mia sita **(Shs 600,000,000/=)** kunakofanywa na baadhi ya watumishi wa Halmashauri hiyo

kupitia mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa mfumo wa 'Point of Sale' **(POS)**

Ndugu wanahabari,

Kufuatia kupokelewa kwa taarifa hiyo uchunguzi wa kina ulianzishwa mara moja, ambapo tuliweza kubaini kuwa kiasi cha shilingi milioni mia sita arobaini na tano mia mbili kumi na nne mia tatu hamsini **(Shs 645,214,350/=)** kilikuwa kimeibiwa na au kufanyiwa ubadhilifu na baadhi ya watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo katika kipindi cha kuanzia Julai 2018 hadi Juni 2020 wasiokuwa waadilifu ambao kwa makusudi waliamua kuhujumu mapato hayo kwa maslahi yao binafsi.

Ndugu wanahabari,

Leo tunapenda kuufahamisha umma wa watanzania kuwa katika uchunguzi wetu hadi leo tumeweza kufanikisha kurejeshwa kwa Jumla ya shilingi milioni mia moja kumi na saba mia tano thelathini elfu mia sita **(Shs 117,530,600/=)** kutoka kwa baadhi ya watumishi ambao waliweza kurejesha fedha hizo na kiasi hiki cha fedha tayari kimekabidhiwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo.

Ndugu wanahabari,

Sanjari na kuwezesha urejeshwaji wa kiasi hicho cha fedha, leo hii tunatarajia kuwafikisha Mahakamani watumishi kumi na mbili kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo kwa makosa ya wizi, ubadhilifu na ufujaji wa fedha za Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo. Watumishi hawa wanatuhumiwa kuiibia Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo Jumla ya shilingi milioni mia nne kumi na nane mia nne themanini na tatu elfu, mia mbili sabini **(Shs 418,483,270/=)**

Ndugu wanahabari,

Watumishi tunaotarajia kuwafikisha mahakamani katika Mahakama ya Wilaya ya Biharamulo leo hii ni hawa wafuatao;-

I. **Shakiru Balyalemwa Sued** ambaye ni Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Ngararambe anayetuhumiwa kuiba/kufanya ufujaji wa Jumla ya shilingi milioni tisa laki mbili thelathini na nane mia moja **(Shs 9,238,100/=)** mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo

II. **Joyce Deusdedith Nkuba** ambaye ni Afisa Kilimo Kata ya Kaniha anayetuhumiwa kuiba/kufanya ufujaji wa Jumla ya shilingi milioni tatu laki nneelfu sabini na nne mia nne **(Shs 3,474,400/=)** mali ya Halmashauri ya wiaya ya Biharamulo

III. **Allen Rwiza** ambaye ni Afisa Mtendaji wa Kata ya Lusahunga anayetuhumiwa kuiba/kufanya ufujaji wa Jumla ya shilingi milioni sitini laki tatu elfu tisini na saba mia sita **(Shs 60,397,600/=)** mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo

IV. **Theresia Kundi Nicodemo** ambaye ni Afisa Mhudumu wa afya katika ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya ya Biharamulo anayetuhumiwa kuiba/kufanya ufujaji wa Jumla ya shilingi milioni thelathini na mbili laki tano tisini na nne elfu mia mbili hamsini **(Shs 32,594,250/=)** mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo

V. **Godeliva Matimba Karantini** ambaye ni Afisa Afya Biharamulo mjini anayetuhumiwa kuiba/kufanya ufujaji wa Jumla ya shilingi milioni kumi na saba laki tisa elfu sabini na tisa mia tisa ishirini **(Shs 17,979,920/=)** mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo

VI. **Salanga Matesi Mahendeka** ambaye ni Mhasibu wa Mapato Halmashauri Biharamulo anayetuhumiwa kuiba/kufanya ufujaji wa Jumla ya shilingi milioni thelathini na tatu na elfu ishirini na sita mia tano **(Shs 33,026,500/=)** mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo

VII. **James Nzihekele Ndibwile** ambaye ni Afisa Mtendaji wa Kijiji Kasato anayetuhumiwa kuiba/kufanya ufujaji wa Jumla ya shilingi milioni **(Shs 23,554,300/=)** mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo

VIII. **Revocatus Kihama Mwesiga na Allen Rwiza ,** ambao ni Afisa Mtendaji wa Kata ya Biharamulo Mjini na Lusahunga wanaotuhumiwa kuiba/kufanya ufujaji wa Jumla ya shilingi milioni thelathini na tisa laki tisa sitini na moja elfu mia tano **(Shs 39,961,500/=)** mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo

IX. **Jeremia Kasaiza** ambaye ni Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Nyakanazi anayetuhumiwa kuiba/kufanya ufujaji wa Jumla ya shilingi milioni themanini na tatu laki moja tisini na nane elfu mia tano **(Shs 83,195,500/=)** mali ya Halmashauri ya ~~Wilaya~~ ya Biharamulo

X. **Christian Magorwa** ambaye ni Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Kaniha anayetuhumiwa kuiba/kufanya ufujaji wa Jumla ya shilingi milioni tisini na tano laki tatu elfu kumi na tisa mia saba **(Shs 95,319,700/=)** mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo

XI. **Gilimoni Gilbet Msengi** ambaye ni Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Rusabya anayetuhumiwa kuiba/kufanya ufujaji wa Jumla ya shilingi

milioni kumi na tisa laki saba elfu arobaini na moja mia tano **(Shs 19,741,500/=)** mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo

Ndugu wanahabari

Pamoja na kuwafikisha watumishi hawa mahakamani kwa makosa ya wizi, ubadhilifu na ufujaji wa Jumla ya shilingi milioni mia nne kumi na nane mia nne themanini na tatu elfu, mia mbili sabini **(Shs 418,483,270/=) na kuokoa Jumla ya shilingi** milioni mia moja kumi na saba mia tano thelathini elfu mia sita **(Shs 117,530,600/=)** bado tunaendelea kukamilisha chunguzi zingine zenye Jumla ya shilingi milioni mia moja na tisa laki mbili elfu mia nne themanini **(Shs 109,200 480/=)** ili kukamilisha uchunguzi wa kiasi chote ambacho ni shilingi milioni mia sita arobaini na tano mia mbili kumi na nne mia tatu hamsini **(Shs 645,214,350/=)** kilichoibiwa na kufanyiwa ubadhilifu katika Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo kupitia mfumo wa ukusanyaji mapato ya ndani kwa mfumo wa 'Point of Sale' **(POS)**

Ndugu wanahabari

Pamoja na kuendelea na kukamilisha chunguzi hizi pia tunatarajia kuanzisha uchunguzi mwingine kwa ajili ya kufuatilia mapato ya Halmashauri hii na halmashauri zote za mkoa wa Kagera kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa Julai **2020/ Juni 2021**.

WITO

Tunatoa wito kwa wananchi wote wa Mkoa wa Kagera kushirikiana na TAKUKURU na Serikali kwa ujumla katika mapambano dhidhi ya Rushwa kwani Rushwa husababisha uvunjifu wa haki za binadamu na kumong'onyoa imani ya Wananchi kwa Serikali yao pia hudhoofisha maendeleo.

Niwaombe wananchi wenzangu wa mkoa huu kujiepusha na na vitendo vya rushwa kwani rushwa ni chanzo kikibwa cha umaskini na pia inaweza ikasababisha mafarakano miongoni mwa jamii.

Imeandaliwa na

SIGNED

JOHN K.E JOSEPH

Mkuu wa TAKUKURU MKOA